# Biashara ya hewa ukaa inavyowanufaisha Katavi

Na Budoya Nilla

HEWA ya ukaa ni biashara poa na inalipa. Mtu akisikia sentensi hiyo kwa mara ya kwanza anaweza asielewe kitu lakini ukisoma makala haya hadi mwisho, bila shaka utaelewa.

Kazi kubwa unayotakiwa kufanya ili uweze kufanya biashara hii ni kuhifadhi misitu ya asili iliyo katika eneo lako na kutunza mazingira yako, basi. Misitu ya asili ina uwezo mkubwa wa kufyonza na kuhifadhi hewa ukaa na hewa sumu.

Ukiwa na misitu hii, ili ufanikishe hilo lazima uzuie uharibifu kwa maana ya kuhakikisha hakuna ukataji miti hovyo, hakuna kufyeka miti, kuchoma misitu na kuzuia kufanya shughuli zingine hatarishi kwa uhifadhi wa misitu ikiwemo kufyeka misitu kwa ajili ya kufugua mashamba mapya au kuigeuza malisho ya mifugo.

Badala yake matumizi ya misitu yanatakiwa yawe endelevu sambamba na kupanda miti mbali mbali katika maeneo yako. Ukiweza kufanya hayo utakuwa sasa na uhakika wa kuvuna hewa ukaa na kufanya biashara.

Pengine unaweza kujiuliza, je biashara hii ni kama biashara ya mahindi au biashara nyingine? Kwamba mtu anaweza kupanda na kuvuna mahindi na kuuza sokoni? Hapana sivyo.

Katika biashara hii, mhusikia anachotakiwa kufanya ni kuhifadhi misitu ya asili iliyo katika eneo lake, basi.

Kwa hatua hiyo, taasisi ya Carbon Tanzania watamtafutia wateja duniani wanaotoa ruzuku kwa wanaofaya uhifadhi huo.

Biashara hii imeingia katika Mkoa wa Katavi, hususani katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika na tayari wananchi 21,000 katika vijiji vinane walio katika halmashauri hiyo wamenufaika na mradi wa hewa ukaa.

Hii ni baada ya kuivuna na kulipwa kiasi cha shilingi milioni 380 kupitia Carbon Tanzania chini ya mradi uitwao Ntakata Mountains Redd Plus Project.

Wananchi katika wilaya hiyo wamezuia uharibifu wa misitu waliyoihifadhi ili iwasaide kutunza mazingira ikiwemo kufyonza hewa ukaa na hewa sumu iliyo katika anga la nchi yetu na nje ya nchi.

Kutokana na uhifadhi huo, vijiji husika vimevuna jumla ya tani 82,000 za hewa ukaa na kuiuza kwa thamani ya shilingi 250,000,000.




Mwakilishi wa Carbon Tanzania, Frank Kweka akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera hundi yenye thamani ya Sh milioni 225 fedha inayotokana na mauzo ya hewa ya ukaa.



Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera akishiriki upandaji miti kutunza mazingaira.

Pamoja na uvunaji wa tani hizo, mauzo yake hayajafikia hata nusu ya tani 270,000 ambazo bado hazijauzwa.

Tarehe 2/5/2020 na 12/11/2020 kiasi cha Sh milioni 130 zilitolewa kama motisha na wadau mbali mbali wa uhifadhi kwa vijiji kabla ya kupata wateja na vyeti vya uuzaji wa hewa ukaa na kugawanywa kulingana na makubaliano ya mradi.

Makubaliano hayo yanabainisha kuwa asilimia 10 ya fedha zinazopatikana zinaenda kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ili kugharimia shughuli za usimamizi mazingira wakati asilimia 90 zinagawiwa kwenye vijiji vilivyo katika mradi ambao unakadiriwa kuwa na hekta 230 katika msitu wa Tongwe Magharibi.

Fedha hizo zinatarajiwa kutumika katika miradi ya maendelao ya kijamii na kiuchumi kwa wananchi kama vile ujenzi wa madarasa, utengenezaji wa madawati, kujenga vituo vya afya na miradi ya kuwaletea wananchi nishati ya umeme.

Inaelezewa kuwa ikiwa hewa ya ukaa itauzwa kwa wingi na ukamilifu wake uliopo katika misitu ya vijiji hivyo, kuna uwezekano wa vijiji hivyo kulipwa shiligi bilioni sita na hivyo wananchi wanatakiwa kuendelea kuhifadhi misitu na kutunza mazingira. Miti isikatwe ovyo wala kuchomwa, waepuke kilimo cha kuhamahama na ufugaji usiozingatia tija.

Vijiji vilivyonufaika na mauzo ya hewa ukaa ni Lugonesi, Mwese, Lwega na Bujombe. Vijiji vingine vilivyo katika mradi wa mauzo ya hewa ukaa ni Kapanga, Mpembe, Kagunga na Katuma. Baadhi ya vijiji hivyo viko katika Kata ya Mwese, Tarafa ya Mwese na vijiji vingine viko Kata ya Kasekese.

Carbon Tanzania ndio taasisi inayowezesha vijiji hivyo kupata masoko ya hewa ukaa ipatikanayo katika misitu ya hifadhi za vijiji na maeneo ya malisho.

Je, biashara hii ilianzaje? Ilianza baada ya vijiji vinane kuwekwa kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa maana ya kupimwa maeneo yao na kuyatenga kama vile eneo la hifadhi ya misitu, eneo la kilimo, eneo la makazi, mifugo, huduma za jamii na kadhalika.

Yaani wananchi kupitia mkutano wao wa kujiji wanajipangia namna ya kutumia ardhi yao iliyopimwa kwa faida yao.

Matumizi bora ya ardhi ndio chanzo cha mradi wa hewa ya ukaa kwa maana ya kutenga maeneo ya hifadhi ya misitu na kuilida sawia.

Mradi wa Ntakata Mountains Redd Plus Project unalenga kuhifadhi misitu ya asili na kulinda bayoanuai zote muhimu hasa zilizo hatarini kutoweka ikiwemo sokwe.

Mradi pia umejikita katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kutunza vyanzo vya maji, kutunza wanyamapori na kuwawezesha wananchi walio katika vijiji venye uhifadhi wa misitu asili kunufaika na mauzo ya hewa ukaa.

Mashuleni wanafuzi hufundishwa kwamba sisi binadamu hupumua hewa ya ukaa na baadaye hewa hiyo hufyonzwa na miti na kuhifadhiwa kwenye miti na ardhini lakini sisi binadamu huvuta hewa ya oksijeni inayotolewa na mimea.

Mbali na hewa tunayopumua, anga letu limejaa hewa ukaa zinazozalishwa na shughuli mbalimbali za mwanadamu hususani viwanda. Uchomaji wa mimea pia husababisha hewa ukaa kwenda angani kwa njia ya moshi.

Uzalishaji mkubwa wa hewa ukaa (kaboni) angani huchochea athari ya jotogesi na kusababisha mabadiliko ya tabianchi.

Ongezeko la viwango vya hewa ya ukaa na gesi nyingine angani zinazotokana na shughuli za binadamu husababisha pia kiwango cha joto duniani kuongezeka.

Mabadiliko haya yana maana gani? Mabadiliko haya yana maana ya kuongezeka kwa joto duniani, kuwa na misimu ya mvua isiyoaminika, kupata mvua chache au nyingi zinazosababisha mafuriko, utabiri wa majira kuwa mgumu na mvua kunyesha nje ya misimu iliyozoeleka.

Hali hii huleta athari katika kilimo, uzalishaji wa chakula kupungua kwa sababu ya uhaba wa mvua au mafuriko yanayozoa mazao na ongezeko kubwa la joto, milipuko ya magonjwa ya mimea na wadudu waharibifu wa mazao wanaweza kusambaa hata maeneo ambayo awali hawakuwepo.

Ongezeko la joto duniani limesababisha kuyeyuka kwa theluji katika ncha za dunia na kusababisha ongezeko la kima cha maji baharini.

Kimsingi, kasi ya mwanadamu kuongeza hewa ukaa angani ni kubwa kuliko uwezo wa dunia kufyonza gesi hiyo.

Ukataji wa misitu kwa sababu mbalimbali hupunguza uwezo wa ardhi kuhifadhi hewa ya ukaa, tunapochoma mafuta kwa kuendesha magari yetu na wakati mwingine kuzalisha umeme kwa njia ya mafuta pia tunaongeza hewa ukaa angani.

Kwa kuwa kasi ya ongezeko la hewa ukaa angani ni kubwa, kitu ambacho ni hatari kwa maisha ya mwanadamu mintarafu suala la mabadiliko ya tabianchi, wataalamu wamefanya tafiti na kubaini kuwa njia moja wapo katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni uhifadhi wa misitu ya asili.

Misitu ya asili ina uwezo mkubwa wa kutumia hewa ya ukaa na hewa sumu kama chakula chake.

Misitu ya asili iliyopo katika Halmashauri ya Tanganyika ni miongoni mwa misiti iliyo na uwezo wa kuchangia katika suala la kabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Wananchi mkoani Katavi, watanzania na Waafrika kwa ujumla hatuna budi kuhifadhi misitu na kutunza mazingira yetu kwa manufaa yetu na vizazi vilivyo. Tuendelee kutunza mazingira yetu kwa kupanda miti mbali ikiwemo ya matunda kwa ajili matumizi mbambali sambamba na kufyonza hewa ukaa kwa manufaa yetu.

*Mwandishi wa makala haya ni Ofisa Habari Mkuu, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi.*